

WARENO NA KORTI

Mwafrika RIPOTA WETU DAR, Ijumaa.

WARENO WAWILI WA MSUMBIJI, WALIOFIKISHWA KATIKA KORTI YA DAR ES SALAAM KWA MASHTAKA YA KUNINGIA KATIKA JAMHURI YA TANGANYIKA KWA NJIA ISIYO YA HALALI, LEO WAMEACHILIWA NA HAKIMU, BW. D.J. SNOXALL.

Wareno hao, Jacinto Soares Veloso na Joao dos Santos Ferreira, wakiwa na silaha, waliingia katika Tanganyika kwa ndege ya kivita kutoka Msumbiji; na wakatua katika uwanja wa Dar es Salaam Machi 12 mwaka huu.

Mara walipotua katika kiwanja, walitiwa nguvuni na askari Polisi wa Tanganyika walioitwa na ofisi inayosi-mamia safari za ndege, baada ya kupokea katika redio maneno yakisema: "Sisi ni watoro wa Kireno, tunataka kutua, tuna silaha."

Walipofikishwa kortini, Wareno hao walikana mashtaka kuwa wameingia katika Jamhuri ya Tanganyika kwa njia isiyo halali. Ila wao wakijitetea, walidai kuwa ni watoro, na wanaomba ulinzi wa kisiasa.

Wareno hao walipofikishwa katika korti leo kwa mara ya tano, Ofisa wa Polisi aliyesimamia mashtaka Bw. S.E. Aesa, alimwambia Hakimu kuwa anaondoa mashtaka kwa Wareno hao kwa kufuata maagizo aliyopewa na Mkurugenzi wa Mashtaka katika Jamhuri ya Tanganyika.

20/4/63
Tunashukuru

Baada ya kuachiliwa huru, Wareno hao wakasema: "Tunashukuru sana Serikali ya Tanganyika. Mungu wetu sasa yu nasi Dar es Salaam." Lakini walikataa kusema kwa nini walitoroka Ureno; ilaralisema: "Tutawaambieni baadaye, lakini hatunui kurudi Msumbiji."

Alipoulizwa msemaji wa Serikali kama Wareno wawili hao sasa watapewa ulinzi wa kisiasa, akajibu: "Hakuna la kusema."

Inasadikiwa kuwa baada ya kuachiliwa Wareno hao

walikwenda kwenye Makao Makuu ya Frelimo Umoja wa wananchi wa Msumbiji.

Hapo kwanza kesi hiyo iliwahi kuahirishwa mara nne na wakati huo wote Wareno hao walikuwa wanakaa rumande.

Kisa cha kuahirisha kesi hiyo mara nne, ni maombi ya upande wa mashtaka kuwa upelelezi kuhusu Wareno hao unaendeshwa nchini na nje ili kupata ushahisi zaidi.

Kesi ilipoahirishwa mara ya mwisho, Mkurugenzi wa mashtaka katika Jamhuri ya Tanganyika aliwahi kusema kuwa upelelezi huo uliokuwa ukiendeshwa henda ukaleta mashtaka makubwa kuliko hayo waliyofanyiwa.

Hata hivyo, wakati huo wote, Wareno hao walikuwa wanakana mashtaka na kudai wao ni watoro wamekuja Tanganyika kusemia wananchi wa Msumbiji kupigania uhuru wao.